

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO CHA UALIMU BUTIMBA

**MAAGIZO KWA WANACHUO WA STASHAHADA MWAKA WA PILI MUHULA WA
KWANZA TAREHE 01/08/2019**

ADA YA CHUO:

Ada ya Chuo ni **450, 000/=** kwa mwaka. Ada hii inaweza kulipwa kwa awamu mbili yaani **225, 000/=** kwa muhula au unaweza kulipa kiasi chote **450, 000/=** kwa mwaka.

Ada ilipwe baada ya kupata namba ya kumbukumbu (Control number) toka kwa mhasibu wa chuo ndugu Makuru Mohamedi Temambele (0786 441 736).

Ada ya Mtihani wa Taifa (NECTA) shilingi **50,000.00** pamoja na michango mingine ilipwe kwenye akaunti ya michango ya chuo **NMB A/C No. 31101200023** Jina Butimba Teachers Training College.

MICHANGO MINGINE YA CHUO:

S/ N	MCHANGO	KIASI	MAONI
1	Serikali ya wanachuo (SEWABU)	5,000	Kwa mwaka
2	Huduma ya kwanza	10,000	Kwa mwaka
3	Usafi na mazingira	20,000	Kwa mwaka
4	Kukodisha godoro	10,000	Kwa mwaka
5	Michezo	30,000	Kwa mwaka
6	Ulinzi	30,000	Kwa mwaka
7	Ukarabati	25,000	Kwa mwaka
	JUMLA	130,000.00	


MUHIMU SANA:

Mwanachuo aje na **'Bank Pay in Slip'** au Stakabadhi inayotolewa na Benki husika. Unatakiwa uje na *Stakabadhi/Pay in Slip* mbili, moja inayonyesha malipo ya ada ya chuo na nyingine ionyeshe michango mingine ya chuo. Ukichanganya malipo hayo hutarudishiwa fedha yako na itakubidi ulipe mara mbili (fanya malipo sahihi kwenye akaunti husika). Vilevile, stakabadhi za malipo zioneshe jina kamili la mwanachuo husika.

Inashauriwa uwe na kadi ya bima ya Afya kwa ajili ya uhakika wa huduma ya matibabu kutoka katika hospitali yoyote na mahali popote utakapokuwa.

Ujapo chuoni uje na Bunda (01) la karatasi (DOUBLE A, NOPA, SMART COPY) na iwapo unadaiwa ada, michango au kifaa chochote kwa mwaka wa kwanza hakikisha unakamilisha.

Unatakiwa kuja na koti rangi nyeusi yenye mfanano na suruali au sketi yako ya sare ya chuo.


MR. HURUMA E. MAGENI

MKUU WA CHUO WA CHUO

CHUO CHA UALIMU BUTIMBA

Nakala 3. Mwenyekiti wa Bodi ya ushauri ya Chuo cha ualimu Butimba